## TANGAZO LA ZABUNI TAREHE 07 MACHI, 2019

## BODI YA SHULE YA SEKONDARI IJANIJA INATANGAZA KAZI YA UMALIZIAJI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA.

Shule ya Sekondari Ijanija imepata Fedha kutoka Mpango wa EP4R kwa ajili ya umaliziaji wa vyumba 2 vya Madarasa. Bodi ya shule imeamua kwamba Fedha hizo zitumike kulipa Mafundi wenye uwezo wa kufanya kazi za umaliziaji kwa mujibu wa makisio yaliyoainishwa kwenye BoQ.

Bodi ya Shule kwa niaba ya Halmashauri ya Mji Nzega inaalika mafundi wenye uwezo wa kufanya kazi hizo kuwasilisha maombi yaliyojazwa Bei kwa kila hatua ya kazi. Mafundi wanaohitajika ni kama ifuatavyo: -

1. Mafundi wa kumalizia vyumba viwili vya madarasa.
2. Mafundi wa kutengeneza madirisha ya vyuma (grill).
3. Mafundi wa kutengeneza madirisha ya alluminium.
4. Mafundi wa kutengeneza na kufunga fremu na topu za milango.

Maombi hayo yawasilishwe yakiwa yamefungwa kwenye Bahasha. Maombi yatakayowasilishwa yawe na Nakala halisi moja na nakala kivuli [Copy] mbili zikiwa zimejazwa vizuri na kufungwa kwenye bahasha itakayokuwa imeandikwa kazi aliyoiomba. Maombi hayo yawasilishwe Ofisi ya Mkuu wa shule ya Sekondari Ijanija Kata ya Ijanija.

Kwa Mafundi wenye nia ya Kufanya Kazi hii, Nakala za maombi [BoQ, Michoro na Vigezo vya Ubora] Vinapatikana Ofisi ya Mkuu wa shule ya Sekondari Ijanija Kata ya UIjanija. kwa Gharama isiyorudishwa [Nonrefundable fee] ya Tshs. 30,000.00. Malipo haya yalipwe Taslimu [Cash Payment] kwa Mkuu wa shule ya Sekondari Ijanija Kata ya Ijanija.

Mwisho wa kuwasilisha maombi haya ni siku ya Alhamisi tarehe 14 Machi 2019 saa 4.00 Asubuhi. Maombi haya yatafunguliwa kwa uwazi na kwa uwepo wa Waombaji au wawakilishi watakaoona ni muhimu kushiriki ufunguzi huo katika ofisi ya Mkuu wa shule ya Sekondari Ijanija Kata ya Ijanija, Alhamisi tarehe 14 Machi 2019 saa 4:00 asubuhi.

Mwombaji atakayechaguliwa kufanya kazi hiyo atajulishwa kwa Barua kwa ajili ya kujaza Mkataba na kuanza Kazi.

Maombi yatakayochelewa hayatapokelewa na hayatafikiriwa kwa ajili ya kupewa kazi hiyo.

**Mkuu wa Shule**
Shule ya Sekondari Ijanija.

HEADMISTRESS
IJANIJA SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 2...
NZEGA.

JIPYA JIPYA

# OFISI YA MTENDAJI KATA YA WELA

SHULE YA SEKONDARI WELA,

S.L.P. 316,

**NZEGA.**

Tarehe: 11/03/2019

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA ZABUNI KWA AJILI UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA HADI HATUA YA KUPAUWA.**

1. Shule ya sekondari WELA imepokea fedha toka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili hadi usawa wa kupauwa katika shule ya sekondari WELA.
2. Ujenzi wa Majengo hayo utafanyika kwa utaratibu wa kutumia "Force Account" Fundi wenyeji.
3. Mkuu wa Shule ya sekondari WELA anawatangazia Mafundi wote wa ujenzi wenye uwezo wa kujenga Madarasa hayo kuomba kazi ya kujenga madarasa tajwa hapo juu.
   Waombaji/Mafundi watatakiwa kuonyesha kazi ambazo wamewahi kuzifanya pamoja na namba za simu za wateja wao waliowafanyia kazi hizo katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita.
4. Michoro ya Majengo hayo inapatikana kwenye ofisi ya idara ya ujenzi makao makuu ya Ofisi za Halmshauri ya Wilaya ya Nzega kwa ajili ya rejea kabla ya kujaza bei. Kwa mawasiliano zaidi unaweza kupiga simu namba **0765825533 au 0782291637** kwa ufafanuzi zaidi.
5. Mafundi watachaguliwa kwa kuzingatia sifa walizoambatanisha, gharama za ufundi pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za Ununuzi wa Umma.
6. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 15.03.2019 siku ya Ijumaa saa nne kamili asubuhi. Maombi yote yatumwe katika Ofisi ya Mkuu wa shule ya sekondari WELA kwa anuani ifuatayo:-
   KATIBU WA KAMATI YA UJENZI,
   SHULE YA SEKONDARI WELA,
   S.L.P 316,
   **NZEGA/TABORA.**
7. Maombi ambayo hayatapokelewa au kuchelewa baada ya muda tajwa hapo juu , hayatafikiriwa kupewa kazi.

……Tkachinde……

THEOPISTA KACHINDE

MKUU WA SHULE

**NZEGA**

HEAD… …RESS WELA SEC… …RY SCHOOL P.O. BOX 316-NZEGA

JIRA

# TANGAZO LA KAZI ZA UJENZI

Tarehe: 09/03/2019

## TANGAZO LA ZABUNI KWA AJILI YA MAFUNDI WAKUKAMILISHA WA UJENZI WA CHOO CHA SHULE KATIKA SHULE YA SEKONDARI ITOBO

Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imepokea fedha toka Serikali kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa choo cha shule katika shule ya sekondari Itobo kwa mwaka wa fedha 2018-2019

Kamati ya ujenzi ya shule ya sekondari Itobo inawatangazia Mafundi wote wa ujenzi wenye uwezo wa kukamilisha ujenzi wa choo hicho kuomba kazi ya kukamilisha choo hicho Halmashauri ya Wilaya ya Nzega katika shule ya sekondari Itobo.

Ukamilishaji wa vyumba hivyo hilo utafanyika kwa utaratibu wa kutumia "Force Account".

**Sifa za mwombaji:-**

a. Muombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo yanayofanana na kazi anayoomba (majengo ya serikali yatakuwa na faida zaidi) mwenye uangalizi mzuri wa mali wakati wa utekelezaji wa mradi huo.
b. Muombaji ajue vyema kusoma ramani na vipimo vyake kwa ajili ya ufanisi wa kazi
c. Muombaji aonyeshe mchanganuo wa muda wa utekelezaji mradi.
d. Maombi yataendelea kuwa hai kwa muda wa siku **45** baada ya kufunguliwa.
e. Muombaji awe na akaunti benki itakayowezesha malipo kwa njia ya hundi
f. Kuwa na cheti cha ufundi ni sifa ya ziada.
g. Muombaji awe na barua ya utambulisho wa eneo analotoka
h. Muombaji awe na barua ya mdhamini kwa kazi husika

i. Waombaji/Mafundi watatakiwa kuonesha kazi ambaz wamewahi kuzifanya pamoja na namba za simu za wateja wa waliowafanyia kazi hizo katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita.

Aidha kila mwombaji atatakiwa kuonyesha gharama za ufundi za ukamilishaji wa choo hicho. Mchanganuo wa kazi hiyo utaukuta shuleni.

Mafundi watachaguliwa kwa kuzingatia sifa walizoambatanisha, gharama za ufundi pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za Ununuzi wa Umma.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20 Machi, 2019 saa saba kamili mchana na waombaji wote wanatakiwa wawepo.** Maombi yatakayochelewa baada ya muda tajwa hapo juu hayatapokelewa kwa ajili ya tathmini. Ufunguzi wa zabuni utafanyika mara baada ya muda wa kupokea zabuni kuisha.

Maombi yote yatumwe katika Ofisi ya Mkuu wa Shule, Shule ya Sekondari Itobo kwa anuani Ifuatayo:-

MKUU WA SHULE,
SEKONDARI YA ITOBO,
S. L. P 540,
**ITOBO, NZEGA.**

**Gharama za maombi hayo ni shilingi 10,000.00 (elfu ishirini tu) ambazo hazitarudishwa.**

**Imeandaliwa na;**

……………………

**BENSON M. JOHNSON**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI ITOBO**
**NZEGA**

HEADMASTER
ITOBO SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 540
NZEGA